
# WALIMWENGU NA MAASI

C . Mzena
Dodoma Cathedral
2006






1. Nuru i mekuja jama, ulimwenguni
   Imeletwa kwetu kumfu, kuza shetani
   Lakini walimwengu hawaitaki
   Wanavyoichukia haisemeki
   Wapenda giza badala ya mwanga
   Lakini walimwengu hawaitaki wanavyo
   Ichukia haisemeki, wapenda giza
   Badala ya mwanga.

2. Injili imeenea dunia nzima
   Na watu wamesikia habari njema
   lakini cha ajabu yaonekana
   Madhambi ndiyo kwanza yazidi sana
   Maasi yatendeka bila woga x 2.

3. Neno la Mungu pote limeshaenea
   Kwa lugha zote neno limetufikia
   watu wasikiliza na kulibeza
   Na makufuru tele wayaeneza
   Ee Yesu shuka kwetu kutuchunga x 2.

4. Watu sasa Mungu wao ni Mungu pesa
   Mwingi wa kutukuka ndiye anasa
   Watu hapo hawashikiki kabisa
   Mungu wa kweli mbali wamemtosa
   Ufisadi unavaliwa njuga x 2.

5. Ni maasi kwenda mbele hii dunia
   Watu sasa ndiyo wanayafagilia
   Ibada hawataki kuzisikia
   Na mahubiri watu wayachukia
   Ukengeufu umeshatusonga x 2.